

Sisi Ni Nani

Montana Fair Housing ni shirika la kibinafsi, linalotoa huduma kamili, lisilo la faida ambalo limejitolea kukomesha ubaguzi wa makazi.

Wito Wetu

Kukuza na kuhakikisha kutobaguliwa ndani ya Montana kuitia uhamasishaji, elimu, utatuzi wa migogoro na utekelezaji.

Jinsi UNAVYOWEZA Kusaidia

Ikiwa ungependa kutoa mchango kwa Montana Fair Housing, chanaua tu msimbo huu ili kufikia sehemu ya mchango kwenye tovuti yetu!



Donate to MFH

Wasiliana

Ili kuripoti ubaguzi wa makazi au ikiwa una maswali kuhusu sheria za nchi, jimbo, au za eneo lako zinazohitaji makazi kupatikana kwa msingi wa nafasi sawa, wasiliana na Montana Fair Housing.



Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili ilifadiliwa na ufadili chini ya ruzuku ya Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mijini ya Marekani. Ni mwandishi na mchapishaji pekee wanaowajibikia usahihi wa taarifa na ufasiri ulio katika chapisho hili. Ufasiri huo sio lazima uwe unaonyesha maoni ya Serikali ya Nchi.

Machi 2022

Shiriki

Tuna nafasi za wafanyakazi wa kujitolea zinazopatikana! Tuma barua pepe kwa inquiry@montanafairhousing.org au upige simu ili kubainisha jinsi unavyoweza kutusaidia kumaliza ubaguzi wa makazi.



Kuhimiza Nafasi Sawa za Makazi Kote Montana

**501 East Front Street, Suite 533
Butte, MT 59701**

Sauti: (406) 782-2573

Faksi: (406) 782-2781

**Bila Kutozwa Ada:
(800) 929-2611**

**Huduma ya Relay ya
Montana: 711**

Barua Pepe:

inquiry@montanafairhousing.org

Tovuti:

www.montanafairhousing.org

Muundo Mbadala
Unapatikana Unapoombwa

Makazi ya Haki—Ni Haki Yako Na Ni Sheria

Sheria za Haki za Makazi hukulinda dhidi ya kutishiwa, kulazimishwa na kunyanyaswa.

Endapo utawasilisha lalamiko kuhusu ubaguzi wa makazi, sheria za nchi na jimbo za Makazi ya Haki zinakataza kulipiza kisasi.

Kuanzia Februari 2021, HUD itachunguza malalamiko yaliyo chini ya mamlaka yake kuhusu ubaguzi kwa msingi wa jinsia ambayo yanajumuisha madai yanayotokana na utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kingono.

Ubaguzi hufanyika mtoe huduma wa makazi anapofanya uamuvi kuhusu ustahiki wa familia wa kupata huduma, au anapotumia sheria na/au masharti tofauti kwa familia, **KWA SABABU YA** ushiriki wa familia katika tabaka linalolindwa, au hali ya tabaka linalolindwa ya mtu anayehusishwa na familia hiyo.

Matabaka Yanayolindwa na Nchi:

- Umbari
- Rangi
- Dini
- Asili ya Kitaifa
- Jinsia (ni pamoja na mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia)
- Ulemavu
- Hali ya Familia

Matabaka ya Ziada Yanayolindwa na Jimbo:

- Hali ya Ndoa
- Imani
- Umri

Sheria za eneo lako zinaweza kutoa ulinzi wa ziada.

Sheria ya Nchi ya Makazi ya Haki na Sheria ya Haki za Kibinadamu ya Montana hairuhusu ubaguzi wa makazi katika huduma zote zinazohusiana na makazi na inatumika kwa mashirika yote. Kuna baadhi ya hali zisizofuata kanuni za kawaida.

TUNACHOFANYA

Huduma:

- Uhamasishaji wa watoa huduma, mawakili na watumiaji wa huduma ili kuhakikisha wanafahamu sheria za kutobagua
- Nafasi za elimu kwa watoa huduma wa makazi, watumiaji wa huduma na mawakili
- Huduma za utatuzi wa migogoro ili kushughulikia matatizo yanayohusiana na sheria za kutobagua za nchi, jimbo, na/au za eneo lako, ikiwa wahusika wangependa kusuluhisha matatizo kabla ya kuwasilisha kesi rasmi ya kisheria.

Utekelezaji:

- Kupeleleza madai ya ubaguzi na kuwashauri waathiriwa wa ubaguzi wa makazi
- Usaidizi wa kuwasilisha malalamiko ya kiutawala kwa Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mijini, na Ofisi ya Haki za Kibinadamu ya Montana.